



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI
ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA USHETU



Unapojuji tafadhali taja:
Kumb. Na. UDC/L.40/8/48

01 Novemba 2023

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MKATABA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu anawatangazia nafasi za kazi watanzania wote wenye sifa za kuajiriwa kwa mkataba katika nafasi ya Dereva wa Mkataba.

1. DEREVA WA MITAMBO – NAFASI 3

A. Sifa za Mwombaji

1. Awe amehitimu Kidato cha Nne (IV)
2. Awe mwenye leseni ya daraja G ya kuendesha Mitambo
3. Mwenye uzoefu wa kuendesha mitambo kwa muda usiopungua miaka mitatu (3) bila kusababisha ajari.

NB: wenye leseni zenyenye sifa za ziada kama daraja F, E na C1 watapewa kipaumbele.

B. Kazi/Majukumu

1. Kuendesha mitambo
2. Kuhakikisha mtambo unafanyiwa matengenezo kulingana na ratiba
3. Kuhakikisha mtambo, unakuwa katika hali ya usafi na usalama wa mtambo wakati wote.
4. Kufanya matengenezo madogo madogo ya mtambo
5. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na Mwajiri.

C. Mshashara: Ngazi ya Mshahahra wa Serikali (TGS B)


D. Masharti ya kazi: Ajira ya Mkataba wa mwaka mmoja.

E. Vigezo na Masharti ya Jumla kwa waombaji.

1. Mwombaji awe raia wa Tanzania
2. Mwombaji awe na umri kati ya miaka 18 hadi 45
3. Mwombaji aambatanishe maelezo binafsi (Detailed CV) yenye anuani ya posta na namba ya simu ya kuaminika ikiambatana na majina ya wadhamini watatu (3)
4. Mwombaji aambatanishe na nakala ya cheti cha kuzaliwa, vyeti vya kuhitimu mafunzo ya uendeshaji wa mitambo,nakala ya Leseni na vyeti vya kidato cha Nne vilivyothibitishwa na Mwanasheria.
5. Mwombaji aambatanishe picha ndogo mbili (2) za rangi (Passport size) ya hivi karibuni.

6. Testimonials, provisional results, Statement of results na hati za matokeo ya kidato cha nne na sita (form IV na form VI) result slips HAITAKUBALIWA.
7. Mwombaji aliyesoma elimu ya kidato cha nne (4) nje ya Tanzania ahakikishe vyeti vyake vimekaguliwa na kuthibitishwa na Mamlaka husika (NECTA).
8. Mwombaji aliyesataafu katika Utumishi wa Umma haruhusiwi kuomba isipokuwa kama na kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
9. Waombaji watakaowasilisha vyeti, na taarifa za kughushi watachukuliwa hatua za kisheria na mamlaka zinazohusika.
10. Waombaji wote waambatanishe Namba ya Utambulisho wa Uraia (*National Identification Number*) kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA). Utambulisho huo uwe umethibitishwa na Afisa Usajili Wilaya, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).
11. Maombi yote yaandikwe kwa mkono na kwa lugha ya Kiswahili.
12. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni siku ya Jumanne, tarehe 14 Novemba 2023, saa 09:30 Alasiri.
13. Maombi yote yatumwe kwa njia ya posta kupitia anuani ifuatayo;

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu,
S. L. P 50,
KAHAMA.



NAKALA: Katibu Tawala (M),
S. L.P 320,
SHINYANGA.

Katibu Tawala (W),
S.L.P 01,
KAHAMA.

Mbao zote za Matangazo,
Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu, Msalala na Manispaa ya Kahama.
KAHAMA.